

WATETEZI KATIKA DINI:

Uzazi wa Mpango katika Pwani ya Kenya



KMYDO

KENYA MUSLIM
YOUTH DEVELOPMENT
ORGANIZATION

UTANGULIZI

Zaidi ya nusu ya wasichana wote waliobalekh au waliovunja ungo wanaoshiriki ngono nchini Kenya wanataka kukawiza ujauzito lakini hawatumii njia za kupanga uzazi.^{1,2} Japokuwa serikali kuu imejitolea kupunguza viwango vya ujauzito kwa vijana na kutoa sera ya afya ya uzazi ya vijana walio vunja ungo, mkoa wa pwani umekuwa na maendeleo



madogo. Lakini hali hii imeanza kubadilika kutokana na ushirikiano kati ya asasi za kiraia (CSOs)—ikijumuisha Shirika la Maendeleo ya Vijana Waislamu wa Kenya (KMYDO)—na maafisa wa serikali za mitaa na maafisa afya kutatua ukosefu wa huduma za afya ya uzazi na raslimali fedha katika eneo hilo. Ushirikiano unaoendelea kati ya asasi za kiraia na serikali ni muhimu katika kuendeleza malengo haya, ikizingatiwa kwamba kuna ripoti zinazoeleza kuwa zaidi ya wasichana wadogo 17,000 walipata ujauzito katika kaunti za pwani nchini mnamo 2018.

KMYDO, shirika la kitaifa la Waislamu linaloongozwa na vijana, limehimiza matumizi ya njia za kupanga uzazi miongoni mwa Waislamu katika kaunti za Kilifi, Lamu, Kwale na Mombasa tangu 2016. KMYDO inakuza uwezo wa maimamu na wafanyakazi wa afya kuelimisha jamii katika kaunti hizi nne kuhusu afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa viongozi wa Kiislamu na majadiliano yanayohusisha watoa huduma juu ya jinsi Uislamu unavyounga mkono uzazi wa mpango. Pamoja na kujenga uwezo, KMYDO imeshirikiana na serikali za mitaa na wadau wengine kutetea sera za uzazi wa mpango zinazolenga vijana, kama vile elimu ifaayo juu ya maswala ya ngono kwa rika mbali mbali, pamoja na raslimali fedha. Matokeo ya kazi hii ya utetezi ni kutengenezwa kwa mipango iliyokasimiwa ya uzazi mpango (CIPs), ambayo ni miongozo kwa Kaunti za Kilifi, Lamu, Kwale na Mombasa katika kupanua huduma za afya ya uzazi kwa vijana. Mipango hii pia inahakikisha miradi na shughuli zinatengewa fedha za utekelezaji. Sasa kwa kuwa mikakati hii imezinduliwa, KMYDO na CSO zingine zinaweza kufanya kazi kwa kushirikiana na watunga sera ili kuifuatilia serikali katika kuleta maendeleo, na kuhakikisha uwajibikaji kwa mkoa kufikia malengo yaliyowekwa.

Katika kipindi cha miaka mitatu hadi sasa ya kufanya kazi katika pwani ya Kenya, KMYDO imehamasisha ushiriki wa vijana vijijini, imeimarisha uongozi mashinani na kuunga mkono uimarishaji wa utetezi wa uzazi wa mpango. Takwimu zifuatazo zinaonyesha baadhi ya watetezi ambao KMYDO imeibua, imewapa mafunzo au kuungana nao ili kukuza uelewa kuhusu uzazi wa mpango na kwa vijana kufikiwa na huduma hizi.

MATOKEO YA AFYA YA NGONO NA UZAZI KWA VIJANA WALIOBALEKH NCHINI KENYA

75%

75% ya idadi jumla ya watu wako chini ya miaka 34.³

20%

20% ya wasichana waliobalekh (wa miaka 15-19) tayari wamezaa au wana mimba ya mtoto wao wa kwanza.⁴

63%

63% ya mimba za utotoni ni zile zisizotarajiwa, na zaidi ya tatu kati ya 10 ya mimba huavywa (hutolewa).⁵

48%

48% ya walioavya mimba na wanaohitaji huduma za afya ni wasichana waliobalekh na wanawake.^{6,7}

40%

40% ya maambukizi mapya ya VVU yamo miongoni mwa vijana (wenye umri kati ya miaka 15-24).⁸

7%

7% ya vituo vyote vya afya hutoa huduma rafiki kwa vijana.⁹

MATOKEO YA UTETEZI WA SERA NA BAJETI



KAUNTI YA KILIFI

- CIP mnamo 2017 kwa kipindi cha miaka mitano (2017-2021).
- Kutengwa bajeti ya KES milioni 5 katika mwaka wa fedha 2016/17, KES milioni 3.5 katika mwaka wa fedha 2017/18, na KES milioni 5.2 katika mwaka wa fedha 2018/19 kwa ajili ya uzazi wa mpango.
- Kuandaa na kuzindua Mkakati wa Afya ya Uzazi na VVU kwa Vijana waliobalekh mnamo 2019 kwa kipindi cha miaka mitano (2019-2022).




KAUNTI YA LAMU

- CIP mnamo 2017 kwa kipindi cha miaka sita (2017-2022).



KAUNTI YA MOMBASA

- CIP mnamo 2018 kwa kipindi cha miaka mitano (2018-2022).
- Kutengwa bajeti ya KES milioni 2.5 katika mwaka wa fedha 2017/18, KES milioni 3 katika mwaka wa fedha 2018/19 kwa ajili ya uzazi wa mpango.
- Kutoa kipaumbele kwa afya ya uzazi katika Mpango Jumuishi wa Maendeleo wa Kaunti mnamo 2018.
- Kuandaa Mkakati wa Afya ya Uzazi na VVU kwa Vijana Waliobalekh mnamo 2019.



KAUNTI YA KWALE

- CIP mnamo 2016 kipindi cha miaka mitano (2016/17-2020/21).
- Kuweka mpango kazi wa kudhibiti mimba za utotoni mnamo 2018.

KULETA JAMII PAMOJA ILI KU

Rashid Osman Swaleh, Imamu anayesimamia madrassa 18 huko Rabai, anajinasibu kama mtezezi wa maswala ya uzazi wa mpango. Haikuwa hivi kila wakati. Hapo zamani aliamini kuwa Uislamu hauruhusu kupanga uzazi. Lakini maoni yake yalibadilika miaka mitatu iliyopita wakati alipokuwa mwenyekiti wa shirika la Waislamu linaloshughulikia Elimu ya Afya (MIHE). “Kama jina linavyoonyesha, tunajaribu kubaini masuala yaliyoeleweka visivyo. Mojawapo ni uzazi wa mpango na jingine linahusu afya ya uzazi likiwemo suala la ngono.” Katika jukumu hili jipya, Imam Rashid alianza kujifunza mengi zaidi ili aweze kuhudumia jamii ya Waislamu vizuri zaidi.

“Nilitembelea KMYDO ili niweze kupanua uelewa wangu kuhusu uzazi wa mpango,” Imam Rashid alisema na kuongeza kuwa “Na kutoka KMYDO ndipo nilipopata uelewa



“Kwa hivyo, tunaingilia kati. Pahali popote, wakati wowote tunapogundua kwamba kuna kundi la watu katika jamii ya Waislamu ambao wanasema kuwa [upangaji uzazi] hauruhusiwi katika Uislamu, tunakuja, na kujaribu kuleta taswira ya kweli kutoka kwa mtazamo wa Kiislamu.”

— *Rashid Osman Swaleh*

kwa mtazamo wa Kiislamu: kwamba uzazi wa mpango ni sehemu muhimu ya Uislamu... Niligundua kuwa yale ambayo tulijaribu kupiga marufuku yalifanyika nyakati za Mtume wetu na pia imeelezewa katika Kuraan Tukufu.”

Alijua kuwa maarifa aliyoyapata yataleta mabadiliko katika jamii yake. Imam Rashid alimwambia Mustafa Asman, Mratibu wa KMYDO wa Rabai, kwamba alitaka viongozi wa Kiislamu ambao anawasimamia wajifunze juu ya mtazamo wa Kiislamu juu ya uzazi wa mpango. Baada ya kusikia haya, Mustafa alijitolea kuandaa semina za kukuza uwezo kwa maimamu na maustadhi. Mara tu viongozi walipoelewa msingi huo wa kidini, Imam Rashid alishirikiana na Mustafa kuwaalika watoa huduma wa afya katika eneo hilo kukutana na kikundi hicho cha viongozi wa Kiislamu. Maimamu walitoka kwenye majadiliano hayo na uelewa bora zaidi wa afya ya uzazi na masuala ya ngono— pamoja na mtalaa wa elimu ya ujinsia uliotumika katika kufundisha kwenye madrassa—na watoa huduma za afya (wauguzi) walijifunza juu ya mtazamo chanya wa dini ya Kiislamu kuhusu uzazi wa mpango. Imam Rashid ameendelea kuandaa mikutano hii ili familia ndani ya jamii zipate taarifa, iwe katika msikiti au kliniki za afya.

Imam Rashid anajivunia kwamba “katika eneo hili, maimamu wetu wako mbele zaidi ya maimamu wengine... [wengi wao] sasa wanaelewa juu ya uzazi wa mpango na masuala ya afya ya uzazi” ikilinganishwa na wale ambao bado hawajapata mafunzo kutoka kwa watoa huduma za afya yaliyoandaliwa na KMYDO. Lakini hataiona kazi yake imekuwa ya mafanikio hadi pale ambapo viongozi wote wa Kiislamu katika eneo hilo—haswa wale wanaoishi katika maeneo ya pembezoni wanafikiwa na mafunzo haya kupitia mabingwa wa uzazi wa mpango.

UJIGANIA UZAZI WA MPANGO



“Sikuwahi kupata maarifa kuhusu vizuia mimba. Sikuwahi kuwa na mtu wa kunifundisha au kuniwezesha... [Sasa,] ninashiriki kisa changu... Kwa sababu hakuna hisia bora zaidi kuliko kumsaidia mtu anayehitaji.” — Sylvian Musau

“Mtoto wangu ni Chelsea Daniella. Ana umri wa miezi tisa.” Huku akiwa amemshikilia binti yake kwa karibu, Sylvian anaanza kusimulia mkasa ambao ameshaelezea mara nyingi kwa matumaini kwamba unaweza kubadilisha maisha ya msichana mwingine.

Sylvian alikuwa hajawahi kusikia kuhusu uzazi wa mpango hadi alipobeba ujauzito bila kutarajia alipokuwa na umri wa miaka 20. “Sikujua jinsi gani ya kuwakabili wazazi wangu kwa sababu tayari nilijiona kuwa mtu niliyeshindwa—niliye wahuzunisha.” Sylvian alilazimika kukabiliana si tu na wazazi wake kwani mimba yake ilikuwa ni kitendo cha aibu katika jamii ya Jomvu, na alijua kuwa shutuma hiyo haitakwisha hata baada ya kujifungua. “Kwa hivyo, hujui cha kufanya. Je utoe (uavye) mimba, unamtunze mtoto? Utawezaje? Utamleaje mtoto huyo?”

Ilikuwa ni baada ya kutoka nyumbani ndipo Sylvian alitambulishwa kwa Mtandao wa Vijana wa Pwani, mmoja wa wadau wa mashinani wa KMYDO unaoongozwa na vijana. Wafanyakazi wa matandao huo walimfundisha

Sylvian kuhusu mbinu za kuzuia mimba na uwezeshaji wa wanawake katika wakati wote wa ujauzito wake. Mara tu binti yake alipozaliwa, Sylvian aliamua kuzungumza waziwazi juu ya uzoefu wake ili kusaidia kupunguza unyanyapaa ambao alikabiliana nao. “Ni lazima nishiriki katika kuelezea hadithi au mkasa huu ... Na ninaiona kama inaniimarisha.”

Sasa akiwa na umri wa miaka 21, Sylvian hajishughulishi na kazi za kuwa mama tu bali pia anatoa ushauri kwa wasichana wa miaka 9 hadi 24 kwenye kilabu ya wasichana ambao tayari wana watoto. “Kwa kweli unaona kuwa wengi wao, ni akina mama wadogo... [kutokana na] ngono ya mapema na isiyo salama.” Sylvian anapokea msaada kutoka kwa Mtandao wa Vijana wa Pwani na KMYDO ili kuweza kuwafikishia wasichana wengine wa kaunti ya Mombasa habari juu ya mbinu za kuzuia mimba kama vile kondomu ambayo huzuia maambukizi ya VVU pamoja na ujauzito. Sylvian anatumai kwamba kupitia kwa kazi yake, takwimu za sasa za ujauzito miongoni mwa wasichana zitapungua kwa sababu wanaofikiwa na mkasa wake watahamasika kubadilisha maisha yao.

Muuguzi katika vituo vya afya vya vijijini mashariki mwa Kenya, Kenneth Bundi Miriti ameshuhudia vijana wakiteseka kutokana na kutopata taarifa na uelewa wa maswala ya uzazi wa mpango. Wasichana wenye umri mdogo kama vile miaka 14 walikuja kwenye kliniki yake kujifungua na wakaathirika kwa kupata tatizo la nasuri (fistula). Kenneth alishuhudia wasichana wenye maisha ya kutumainiwa wakifariki wakati wa kujifungua au kutokana na athari za kiafya zitokanazo na uavyaji mimba. Katika kila kituo alichokuwa akihudumia, Kenneth alitenga muda wa kuwataarifu vijana kuhusu chaguzi zao juu ya maswala ya afya ya uzazi pamoja na ngono.

Huku akitabasamu Kenneth anasema, “Hayo ndiyo hunipa motisha, kuona mtu akiishi sehemu kubwa ya maisha yake na kutimiza ndoto zake.” Kama mratibu wa afya ya uzazi na ngono kwa vijana Kilifi, Kenneth sasa anafanya kazi kuhakikisha kuwa vijana katika kaunti hiyo, haswa wasichana na wanawake, kamwe hawatateseka kwa sababu ya ukosefu wa habari au uwezo wa kuchagua.

Baada ya takwimu kuhusu ujauzito miongoni mwa wasichana kutolewa mnamo 2018, Kenneth aliungana na Mustafa Asman, mratibu wa KMYDO, Kilifi, ili kubuni mpango wa kukabiliana na tatizo la mimba za utotoni. “Sio siri kuwa vijana 17,580 (wenye umri wa miaka 15-19) walipata ujauzito mwaka jana... Lakini unapojaribu kuwaambia watu kuwa ni vizuri kuanzisha mbinu za kuzuia mimba miongoni mwa vijana, kama vile kutoa elimu ya ngono, basi unapata upinzani mkubwa,” amesema Kenneth. Yeye pamoja na Mustafa pia walitengeneza mkakati wa afya ya uzazi na ngono kwa vijana wa 2019-2020 ambao ulizinduliwa mnamo Aprili 2019. Mkakati huo unakusudia kupunguza idadi ya mimba za utotoni na kuzuia athari za mila potofu kwa afya ya uzazi kwa vijana. Kaunti ya Kilifi inatenga fedha kwa ajili ya huduma rafiki kwa



“Hii haiwezi kushindwa na mimi kama mtoaji wa huduma ya afya. Inaweza tu kushindwa kwa juhudi za pamoja za kila mmoja, kwa sababu kuna watendaji wengi—wazazi, shule, watunga sera serikalini. Kila mtu, ni lazima tuhusike na tuwe na njia ya kuwaongoza vijana wetu.”

— Kenneth Bundi Miriti

vijana katika vituo vya afya, kutoa mafunzo kwa vijana juu ya kuimarisha, na pia kupunguza ukosekanaji wa dawa za uzazi wa mpango, vyote vikiwa ni jitihada za kufikia malengo ya mkakati huo.

Kilifi itakuwa Kaunti ya nne nchini Kenya kutoa mkakati wa uzazi wa mpango unaolenga vijana. Wakati wa kutengeneza mkakati huo, Kenneth alisisitiza vijana wawe kiini cha mchakato huo—kutokana na hilo, 80% ya wale ambao walihusika walikuwa vijana wa chini ya umri wa miaka 20. “Tulileta asasi za kiraia CSOs ambazo zinaendeshwa na vijana. Tulileta vijana kutoka sehemu mbali mbali. Na wao ndio walichangia kila kipengele kwenye mkakati huu—tuliwaongoza tu katika masuala ya kitaalamu.”

Kenneth anaendelea kutetea huduma kamili ya afya ya uzazi kwa vijana katika kazi zake zote.

Wakati anakua, Maimuna Siraji Twaha hakuwahi kusikia viongozi wa Kiislamu katika jamii yake wakijadili uzazi wa mpango katika misikiti au katika madrasa. Lakini alipofikia umri mkubwa kidogo, alianza kuona wasichana wakiwa wajawazito na kuishia kuwa mama bila kujiandaa. Maimuna akaamua kuvunja ukimya: “Nilichukua hiyo kama fursa... [ya] kuwafundisha wasichana juu ya afya ya uzazi, na ngono. Uzazi wa mpango ni muhimu hata kama kuna shinikizo na ushawishi kutoka kwa marafiki na jamaa.” Maimuna hakuishia hapo. Mtazamo wake—kuwa changamoto yoyote inaweza kugeuzwa ikawa fursa—umemfanya aongoze utetezi wa uzazi wa mpango katika kaunti ya Kilifi.

Kupitia shughuli zake katika Mradi wa Kaloleni, shirika linaloongozwa na vijana linaloandaa vikao vya kuelimisha na kutetea huduma za uzazi wa mpango, Maimuna alikutana na Mustafa Asman wa KMYDO, mratibu wa mkoa wa pwani. Alijadiliana naye akiwa na wazo kwamba, *“Tunahitaji watetezi wengi vijana. Wakati wowote [maafisa wa serikali] wanaponiona, wanajua ninafanya kazi ya afya ya uzazi. Kwa hivyo, je, inawezekana sasa vijana wengine wayazungumzie?”* Kwa pamoja, Mustafa na Maimuna waliwafundisha viongozi wa vijana wa vijijini juu ya jinsi ya kuwasilisha

malengo yao ya utetezi na kukwepa vizuizi ndani ya mchakato wa sera inayolenga watoa maamuzi. Wawili hao walitoa mbinu hizi kwa vijana wakijua kuwa wao ndio wajumbe bora zaidi wa masuala yanayoathiri maisha yao.

Maimuna hutumia stadi hizi kwa njia yake ya kufikisha ujumbe kule waliko vijana. Anaorodhesha malengo yake kwa mpangilio—kuanzisha huduma rafiki kwa vijana katika vituo vya afya, kuunda sera ya jinsia na kuongeza ufadhili kwa kaunti kwenye masuala ya uzazi wa mpango. Kwa kila kazi inayolenga sera, Maimuna anajitahidi kupata utaalamu: “ni lazima uwe na taarifa sahihi mikononi mwako juu ya kwanini, nani na lini.” Hivi karibuni kwa uchunguzi wake mwenyewe, Maimuna aligundua kuwa 80% ya huduma za uzazi wa mpango katika vituo vya afya vya Kilifi zinafadhiliwa na wafadhili. Alileta habari hii kwa watunga sera, akiuliza, “Na je, leo au kesho ufadhili huo ukikosekana?” Utetezi wake stadi ulisababisha kutengwa fungu maalum la fedha kiasi cha dola milioni tatu hadi tano kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Licha ya vizuizi, Maimuna anaendelea kuongeza nguvu katika harakati za utetezi wa uzazi wa mpango miongoni mwa viongozi wa kizazi kijacho, pamoja cha viongozi wanaoshikilia madaraka katika serikali za mitaa.

“Ikiwa utaendelea kushiriki masuala ya afya ya ngono na uzazi na upangaji uzazi, utagundua kuwa wao [jamii] pia wana wazo hilo sasa kwa kuwa wanaweza kuongea juu yake... simama kidete na uwe mtetezi.”

— Maimuna Siraji Twaha



HATUA ZITAKAZOFUATA

KMYDO inaendelea kufanya kazi na mabingwa wa uzazi wa mpango wa pwani kutetea afya ya uzazi na haki za vijana nchini Kenya. Kutokana na kuwashirikisha viongozi wa Kiislamu, watetezi wa vijana na washiriki wa sekta ya afya katika juhudi hii, KMYDO imeleta maendeleo makubwa sio tu katika kaunti za Mombasa, Kwale, Kilifi na Lamu, lakini pia katika kaskazini mashariki mwa Kenya. Katika kaunti ya Nakuru, KMYDO imesaidia katika kutengeneza mfumo kamili wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto pamoja na Vijana, Mpango wa uzazi wa mpango uliokasimiwa wa miaka mitano (2017-2021) na kutetea kutengwa kwa bajeti ya afya ya uzazi. Katika kaunti ya Wajir, KMYDO imesaidia katika CIP ambao ulishirikia watetezi wa katika eneo hilo—kama vile maimamu, wanawake na wazee wa ukoo—ambao wanatoa changamoto kwa mila ya zamani ambazo zilidai kwamba uzazi wa mpango ni haramu, au ni marufuku kutekelezwa.

KMYDO imesonga mbele kwa kupanua kazi hii Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Baraza la Kitaifa la Waislamu wa Tanzania (BAKWATA) na Baraza Kuu la Waislamu wa Uganda (UMSC). Kutokana na hilo, BAKWATA ilitoa maamuzi mawili ya kisheria (Fatwa) mnamo 2019 kuhusu ndoa za utotoni, na pia uzazi wa mpango hususan kipindi kinachostahiki kwa mama kubeba ujauzito baada ya kujifungua. Nchini Uganda, KMYDO itajadiliana na UMSC ili kuhakikisha ahadi za serikali kuhusu uzazi wa mpango zinatimizwa kupitia mtandao wazi wa watetezi katika dini.

HADIDU ZA REJEA

- 1 Shirika la Kitaifa la Takwimu la Kenya, et al. (2015). *Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa Kenya wa 2014*. Imetolewa: <https://dhsprogram.com/pubs/pdf/fr308/fr308.pdf>
- 2 Taasisi ya Guttmacher. (2019). Kufanya Hesabu: Kuwekeza katika Vizuia mimba na Afya ya Mama na Watoto wanaozaliwa kwa Vijana Waliobaleghe nchini Kenya, 2018. Imetolewa: <https://www.guttmacher.org/fact-sheet/adding-it-up-contraception-mnh-adolescents-kenya>
- 3 Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD), Mfuko wa Idadi ya Watu wa Umoja wa Mataifa (UNFPA) na Wakala wa Norwei wa Ushirikiano wa Maendeleo (NORAD). (2015). *Utafiti wa Kitaifa wa Vijana wa 2015*. Imetolewa: <http://www.ncpd.go.ke/wp-content/uploads/2016/11/2015-National-Adolescents-and-Youth-Survey-Preliminary-Report.pdf>
- 4 Shirika la Kitaifa la Takwimu la Kenya, et al. (2015). *Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa Kenya wa 2014*. Imetolewa: <https://dhsprogram.com/pubs/pdf/fr308/fr308.pdf>
- 5 Taasisi ya Guttmacher. (2019). Kufanya Hesabu: Kuwekeza katika Vizuia mimba na Afya ya Mama na Watoto wanaozaliwa kwa Vijana Waliobaleghe nchini Kenya, 2018. Imetolewa: <https://www.guttmacher.org/fact-sheet/adding-it-up-contraception-mnh-adolescents-kenya>
- 6 Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Kenya. (2013). *Matokeo na Matatizo ya Uavyaji Mimba Usio Salama nchini Kenya: Matokeo Muhimu ya Utafiti wa Kitaifa*. Imetolewa: <http://aphrc.org/wp-content/uploads/2013/11/Incidence-and-Complications-of-Unsafe-Abortion-in-Kenya-Key-Findings-of-a-National-Study.pdf>
- 7 Kituo cha Afrika cha Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya. (2014). Uavyaji Mimba Usio salama kati ya Wasichana Waliobaleghe na Wanawake Wachanga nchini Kenya: Hatua ya Haraka Inahitajika. Imetolewa: <http://aphrc.org/wp-content/uploads/2015/02/PAC-policy-brief-final.pdf>
- 8 Baraza la Kitaifa la Kudhibiti Ukimwi. (2018). *Ripoti ya Maendeleo ya Hatua dhidi ya UKIMWI nchini Kenya 2018*. Imetolewa: https://www.lvcthealth.org/wp-content/uploads/2018/11/KARPR-Report_2018.pdf
- 9 Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Kenya. (2016). *Miongozo ya Kitaifa ya Utoaji wa Huduma Zinazowapendeza Vijana nchini Kenya*. Imetolewa: <https://faces.ucsf.edu/sites/faces.ucsf.edu/files/YouthGuidelines2016.pdf>



Shirika la Maendeleo ya
Vijana Waislamu nchini
Kenya (KMYDO)



1300 19th Street NW, Suite 200
Washington, DC 20036-1624 USA
+1 (202) 557-3400 | www.pai.org | info@pai.org

Old Nairobi-Nakuru Road, Section 58
Nakuru, Kenya
+254 707 002 201 | www.kmydo.org | info@kmydo.org